


# Ukweli Juu Ya Kanisa

(The truth about the Church)

UKWELI JUU YA KANISA: MAJULISHO

Tunaishi wakati unao weza kuitwa "Wakati wa Kanisa". Wakati huu, Mungu anatayarisha kundi la watu waitwao Kanisa Lake. Watu hawa pia wanaitwa

wa Kristo, yaani kanisa lake. Yesu ndiye kichwa (kiongozi) wa kanisa lake. "Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe. karna Kristo ni kichwa cha Kanisa. Ni mwili Wake (kanisa) alio uokoa" (Waefeso 5:23) Hí uweze kuokoka ni lazima uwe katika Kanisa.

UNAINGIA **KANISANI JINSI GANI?**

Inakupasa uzaliwe katika Kanisa. Kuzaliwa huku siyo kuie kuzaliwa naye mama yako. Ni lazima uzaliwe mara ya pili. Yesu alimwambia Nikodemu, ni lazima kuzaliwa kwa maji na Roho au atakosa kuuona mji mtakatifu wa Mungu (Yohana 3:5)

Katika Matendo ya Mitume mbili, watu wa kwanza walizaliwa

katika kanisa. "Kwa ghafla kulikúwa nayc sauti kutoka mbinguni kama upepo uendao kasi wenye nguvu. Ukaijaza nyumba yote waliyo kuwemo. Wakaona ndimi zilizogawanyika zilizo onekana kama ndimi za moto. Ndimi hizi zilikuwa juu ya kila mmoja. Wakaanza kunena kwa lugha nyingine kama jinsi Roho Mtakatifu alivyo wajalia kutamnka". (Matendo ya Mitume 2:2-4).

Kulikuwa nao watu mia moja ishirini walio zaliwa katika kanisa. Walakini, watu wengi walijionea mambo yalio kuwa yakiendelea na kuuliza iinsi wawezavvo 'uranya Ui nao pia waweze kuingia katika kanisa. "Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu." (Matendo ya Mitume 2:38).

**UKWELI JUU** YA KANISA:

Watu elfu tatu walitii maneno ya Petro nao wakazaliwa katika kanisa siku He. Mambo haya yalifanyika siku ya Pentekoste (Sherehe ya Kiyahudi) Kanisa liliIo zaliwa siku hiyo tunaliita Kanisa la Kipentekoste.

Mwili uliookolewa wa Kristo, kanisa, iliendelea kukua sana. Liliendelea kukuwa kama jinsi ilivyo kuwa imeahidiwa. "Ahadi hü ni kwenu na kwa watoto wenu. Ni kwa watu wote kila **mahali." Ni kwa** wote watakaoitwa na Bwana Mungu **wamjie". (Matendo ya** Mitume 2:39)

Wewe pia unaweza **kuzaliwa katika** kanisa. Ni lazima uzaliwe tena

kama jinsi waaminio walizaliwa tena katika kanisa. Watu wengine wangetaka kufundisha kwamba kunayo njia nyingine lakini hakuna. La! hakuna aina nyingine ya habari njema. Kunao watu wengine wangependa kukuongoza katika njia isiyo sawa, (Wagalatia 1:7), Mungu anatuonya juu ya walimu wa uwongo na kwamba ni lazima tujihadhari kwamba wasitudanganye.

Biblia inatueleza juu ya watu wengine wengi walio zaliwa katika kanisa kwa njia ya kutubu dhambi zao, kubatizwa katika jina la Yesu, na kujazwa Roho Mtakatifu. Wasamaria **(Matendo ya** Mitume 8), Kornelio na nvumba yake akiwa na rafiki zake (Matendo ya

Mitume 10), nao watu wa Eteso (Matendo 19) walikuwa wachache. Walinena kwa lugha nyingine walipo zaliwa katika kanisa.

Kwa rmida mfuni ilisemwa iuu ya Wakristo (yaani jina lingine la kanisa) kwamba wa(rieljaza yerus:ait..-In na matundisho yau. Baadaye watu walianza kusema kwamba kanisa imegeuzwa juu chini nayo habari njema ya wokovu kupitia Jina la Yesu.

UKWELI JUU YA **KANISA: MATENGENEZO:**

Siyo watu wote wanaelewa maonyo juu ya mafundisho ya uwongo. Wengine basi walianza kufuata mafundisho ya mwanadamu na siyo ya Mungu. VVakadai kwamba wao ni sehemu ya kanisa, lakini walikuwa siyo sehemu. Kanisa la kweli la Yesu Kristo liliendelea kuitwa katika Jina Lake na likaendelea kukaa likiwa limeja✓a na Roho Mtakatifu.

Watu walio amini kwamba ni lazima utubu, ubatiz✓e katika Jina la Yesu, na kunena kwa luaha nyingine ukipokea Roho Mtakatifu, waliteswa. Walakini. waliendelea kushikilia mafundisho ya Biblia. Hawakusikiliza maneno isiyo tokana na watu wa Mungu. Watu wengi walikufa kwa sababu ya kusimamia ukweli,

**KURUDI KWA PENTEKOSTE:**

Mwanzo wa karne hü katika Topeka, Kansas. U.S.A., kulikuwa nalo **kundi la watu walio** zaliwa tena kwa Roho Kama jinsi ilivyo kuwa siku ya Pentekoste, walinena kwa lugha nyingine karna jinsi Mungu aliwajaza na Roho Mtakatifu. Tangu wakati hun watu wengi wamepokea Roho Mtakatifu **wakiwa nayo** ushahidi wa kunena kwa lugha nyingine, kote **ulimwenguni.**

Roho Mtakatifu. **anaye kuja** kuwaongoza watu, kwenye ukweli, **amewaonyesha** watu nawa Kwarnba ni lazima wabatizwe **katika Jina la** Yesu. Hivi ndivyo watu walio zaliwa katika **Kanisa nyakati** za Biblia walibatizwa. Ubatizo katika Jina **la Yesu ilikuwa** sehemu ya mafun-disho ya Petro siku ya Pentekoste. Watu wa Mungu kote ulimwenguni **wanahubiri** ujumbe wote wa wokovu kama jinsi inavyo patikana **katika** Biblia

Katika mwaka **wa** 1945 madhehebu mawili vakiwa yahubiri ujumbe **huu ulio** sawa, yaliungana na kuwa UNITED PENTECOSTAL CHURCH

**UKWELI JUU YA** KANISA:

**Mafundisho yetu** ya msingi ni:

"Mafundisho ya msingi wa kanisa hili ni ule wokovu wa Biblia kwa jumla, **ambayo** ni toba, ubatizo kwenye maji mengi kwa njia ya kuzamishwa katika Jina la Yesu Kristo, na ubatizo wa **Roho** Mtakatifu ikiwa nayo ishara ya kunena kwa luaha nyingine kama iinsi Roho atamjalia mtu kutamka. Tutadumu umoja wa Roho bado tutakapo sote fikia umoja wa imani. Hivyo hivyo, tukiendelea kuonya **wandugu** wote kwamba v✓asiendelee kushindana juu ya tofauti zao kuuacha umoja wa mwili.

KUMALIZA:

"Kwenye mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, Milango ya kuzimu haitalishinda" (Mathayo 16:18), Yesu anaendelea kulijenga kanisa lake. Unaweza kuwa sehemu ya kanisa Lake. Lakini ni lazima uzaliwe tena kama jínsi kanisa **lake la** zamani Illiku✓a.

Wale walio zaliwa katika kanisa na kuishi maisha takatifu kwake Yesu, ndiyo Yesu anakuja kuwachukual na ku✓ageleka mbinguni kuishi pamoja Naye milele na milele.